## Maswali

1. Athalia alifanya nini ili awe malkia?
2. Nani aliokolewa kutoka kwa Athalia?
3. Nani aliokoa Yoashi?
4. Nani alimlinda Yoashi?
5. Alifichwa Hekaluni kwa muda gani?
6. Kuhani Yehoyada alifanya nini Yoashi alipofika umri wa miaka 7?
7. Nini ilifanyika kwa Malkia Athalia?
8. Mfalme Yoashi alifanya nini kwa Hekalu ya Mungu?
9. Mfalme Yoashi alifanya mazuri na kumtumikia Mungu kwa muda gani?
10. Yoashi alifanya nini kiovu sana baada ya kuhani Yehoyada kufariki?
11. Mfalme Yoashi alikufa namna gani?
12. Tunajifunza nini kutoka kwa maisha ya Yoashi?

## Majibu

1. Athalia aliua wana wa kifalme wote.
2. Mtoto Yoashi alihebeshwa kutoka kwa Athalia.
3. Yehosheba alihebesha Yoashi.
4. Yehosheba na kuhani Yehoyada walimlinda Yoashi.
5. Yoashi alifichwa Hekaluni kwa miaka 6.
6. Yoashi alipofika miaka 7, Yehoyada alimtawaza kuwa Mfalme wa Yuda.
7. Amri jeshi wakuu aliua Malkia Athalia.
8. Yoashi alikusanya pesa kutoka kwa watu na akarekebishia Hekalu.
9. Yoashi alifanya mazuri na kumtumikia Mungu kwa muda wenye Yehoyada alikuwa hai.
10. Yoashi aliua Zekaria mwana wa Yehoyada na Yehosheba.
11. Yoashi aliumizwa kwa vita. Wakati alipokuwa ameshindwa, maafisa wake walimua kwa sababu alikuwa ameua mwana wa Yehoyada.
12. Lazima tupate nguvu kutoka kwa Mungu. Lazima tuwe na msimamo kwa njia za Mungu bila kufuata watu wanaoenda njia mbaya.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 2 Mwaka wa 2

# 75 Joashi mfalme mdogo

### Kwa Biblia

2 Mambo ya Nyakati mlango wa 22:9 – 12 na mlango wa 23

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba tunatakiwa kufanya Mungu awe ndiyo nguvu zetu. Tukifuata watu inamaanisha hatuna imani kwa Mungu.

### Somo

Malkia Athalia alikuwa binti wa Mfalme Ahabu aliyekuwa muovu pamoja na mkewe Yezebeli. Ahazia mwana wa Athalia alikuwa mfalme wa Yuda. Ahazia alikuwa mfalme muovu. Alitawala kwa mwaka moja tu na akauawa.



Ahazia alipouawa, Athalia mama yake alitaka kuwa malkia. Athalia naye alikuwa muovu sana. Alizunguka na akauwa wana wa kifalme wote. Aliuwa watu wa familia yake kwa sababu alitaka kuwa malkia.

Lakini kulikuwa na mwana wa Ahazia mdogo. Aliitwa Yoashi. Alikuwa na umri wa mwaka mmoja tu. Yehosheba, mkewe Yehoyada kuhani, alimficha mtoto Yoashi. Alimuiba kutoka kwa wana wa kifalme waliokuwa wanauawa na Malkia Athalia.

Yehosheba alichukua mtoto Yoashi pamoja na aya wake akawaficha kwa chumba chake cha kulala. Yehosheba alikuwa shangaziye mtoto Yoashi. Alimpeleka kwa Hekalu. Yehosheba na kuhani Yehoyada walificha Yoashi kwa Hekalu kwa miaka sita.

Malkia muovu Athalia hakujua kwamba mjukuu wake, Yoashi alikuwa Hekaluni anakua. Wakati Yoashi alikuwa na miaka 7, Yohayada alijipa ujasiri. Aliamini kwa Mungu. Aliamua kwamba ilikuwa wakati mzuri wa kufanya Yoashi awe Mfalme wa Yuda.



Yehoyada alituma amri jeshi wakuu wa nchi yote. Waliwakusanya makuhani, Walawi na wakuu wa Yerusalemu wote. Yehoyada alifanya mipango kwa utaratibu. Ilikuwa jambo la maana kumsaidia Yoashi ahebe Malkia Athalia. Kila kitu kilifanywa kwa siri.

Yehoyada aligawanya Makuhani na Walawi kwa vikundi vitatu ili walinde maeneo tofauti tofauti. Wakuu nao walilinda. Yehoyada alitoa Yoashi mafichoni. Walawi walimzingira wakiwa wameshika mikuki. Yehoyada aliweka taji kwa kichwa cha Mfalme Yoashi. Na kila mtu akapasa sauti akisema, “Mfalme aishi milele!” Makuhani waliimba na kushangilia.

Malkia Athalia aliposikia kelele za nyimbo na kushangilia, alienda Hekaluni kuangalia kilichokuwa kikiendelea. Aliona Mfalme Yoashi amesimama Hekaluni na makuhani walikuwa wakipiga tarumbeta. Hali kila mtu aliimba na kushangilia. Malkia Athalia alipasa sauti akisema, “Fitina! Fitina!” Kuhani Yehoyada aliambia wanajeshi wakuu wamshike Athalia na wamuue. Kwa hivyo Athalia malkia muovu aliuawa na Yoashi akatawazwa kuwa Mfalme. Yoashi alikuwa na umri wa maika saba alipotawazwa na akatawala kwa miaka arobaini.

Yohayada alipea Mfalme Yoashi nakala ya sheria za Mungu na akamfundisha kupenda na kumtumikia Mungu. Yehoyada, Yoashi na watu wote walifanya agano na wakaahidi kumpenda na kumtumikia Mungu. Walivunja vunja hekalu ya Baali yenye Malkia Athalia alikuwa akiabudia mungu wa uongo.



Wakati wa utawala wa Malkia muovu Athalia, Hekalu ya Mungu ilikuwa imevunjwa. Yoashi alipokuwa mkubwa aliamua kurekebisha Hekalu ya Mungu. Mfalme Yoashi alichukua na kuweka kwa sanduku kubwa pesa zote zenye watu walileta kwa Hekalu. Sanduku lilipojaa pesa, Mfalme Yoashi alizipea wajenzi na maseremala ili watengeneze Hekalu ya Mungu.

Mfalme Yoashi alifanya mazuri kwa muda wote kuhani Yehoyada alikuwa hai. Lakini Yehoyada alipokufa, Mfalme Yoashi alianza kusikiliza maneno ya watu wengine. Aliachana na Mungu. Aliongoza watu kuabudu Baali mungu wa uongo tena.

Mungu alituma manabii kuwambia watu wamrudie lakini, Mfalme Yoashi hakuwasikiliza. Zekaria mwana wa Yehoyada alikuwa mjasiri. Aliendea Yoashi na watu wote akawambia kwamba wanatakiwa wamrudie Mungu. Lakini watu hawakutaka na Mfalme Yoashi akaamrisha wamue Zekaria mwana wa kuhani Yehoyada na Yehosheba waliokuwa wazuri kwake na wakaokoa uhai wake. Ni jambo mbaya sana alilofanya.

Jeshi la Washami walikuja na kushinda jeshi la Yuda. Mfalme Yoashi aliumizwa kwa vita. Alirudishwa kwa jumba ya kifalme. Alipokuwa mgonjwa na ameshindwa, baadhi ya maafisa wake walimuua kwa sababu alikuwa amemuua Zekaria mwana wa Yehoyada Kuhani.

Mfalme Yoashi alikuwa mfalme muovu. Alifuata na kuongozwa na kila mtu aliyekuwa na nguvu kumliko. Alifanya kilichokuwa rahisi. Tunatakiwa tupate nguvu kutoka kwa Mungu. Tusifuate wenzetu tu. Tunatakiwa tuwe na imani na nguvu na tusimame na haki na ukweli.